TANGAZO LA SERIKALI NA. 346 la tarehe 03/05/2024

SHERIA YA UCHAGUZI WA RAIS, WABUNGE NA MADIWANI,
(NA. 1 YA MWAKA 2024)

# NOTISI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 49(1)(b))*

NOTISI YA SIKU YA UTEUZI WA WAGOMBEA KWA UCHAGUZI MDOGO WA UBUNGE KATIKA JIMBO LA KWAHANI YA MWAKA 2024

Jina

1. Notisi hii itajulikana kama Notisi ya Siku ya Uteuzi wa Wagombea kwa Uchaguzi Mdogo wa Ubunge Katika Jimbo la Kwahani ya mwaka 2024.

Siku ya uteuzi

2.-(1) Siku ya uteuzi wa wagombea kwa ajili ya uchaguzi mdogo wa Ubunge katika Jimbo la Kwahani itakuwa siku ya Alhamisi tarehe 23 Mei, 2024.

(2) Mtu yeyote anayekusudia kugombea Ubunge kwa mujibu wa Sheria anapaswa kuwasilisha fomu za uteuzi kwa msimamizi wa uchaguzi wa Jimbo la Kwahani siku ya uteuzi, kabla ya saa kumi kamili (10:00) jioni.

Dodoma,
2 Mei, 2024

JACOBS C. M. MWAMBEGELE
*Mwenyekiti Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi*